N16/2/ABSWA/SP1/SWA/TZ0/XX/T

Diploma Programme
Programme du diplôme
Programa del Diploma

# Swahili B – Standard level – Paper 1
# Swahili B – Niveau moyen – Épreuve 1
# Swahili B – Nivel medio – Prueba 1

Friday 4 November 2016 (afternoon)
Vendredi 4 novembre 2016 (après-midi)
Viernes 4 de noviembre de 2016 (tarde)

1 h 30 m

---

**Text booklet – Instructions to candidates**

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for paper 1.
- Answer the questions in the question and answer booklet provided.

**Livret de textes – Instructions destinées aux candidats**

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

**Cuaderno de textos – Instrucciones para los alumnos**

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.

8816 – 2319

5 pages/páginas

© International Baccalaureate Organization 2016

International Baccalaureate
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

https://xtremepape.rs/

**Kifungu A**

# Utalii Na tamaduni Za pwani; Fort Jesus

❶ Huenda kwa wengi, Fort Jesus ni jengo tu la kufurahisha macho, na kwa wengine ni jumba la zamani tu. Lakini, kuna mengi ambayo yamefichika ndani zaidi ya anavyoliona mtu kwa nje. Fort Jesus inapatikana katika mwambao wa pwani, Jiji la Mombasa, Kenya na katika barabara ya Nkrumah, mtaa wa *Old Town*. Historia yake ilianza pale baharia anayejulikana kama Vasco Da Gama kutoka Ureno alipotua Mombasa mwaka 1498. Azma ya safari yake ilikuwa kutafuta njia za biashara kupitia Bahari Hindi. Kama inavyoeleweka, watu kutoka mataifa tofauti walilipenda sana bara Afrika kwa wingi wake wa malighafi.



❷ Licha ya kuwa Vasco Da Gama na Wareno wenzake walitaka kufanya biashara na watu wa pwani, lengo lingine lilikuwa kueneza dini ya Kikristo. Hili halikuwafurahisha watu wa pwani, hasa wa Mombasa ambao tayari walikuwa wa dini ya Kiislamu. Kisha, Waarabu wa Oman walitaka kuwatoza Wareno ushuru, jambo ambalo lilizua vita vikali.

❸ Fort Jesus ilijengwa mwaka 1593 baada ya mfalme wa Ureno kuamrisha ujenzi wake. Jengo lenyewe lilijengwa juu ya jabali na kutumiwa kuilinda bandari, kama ngome ya jeshi kati ya mwaka 1837 hadi 1895 na hatimaye kugeuzwa kuwa jela ya wafungwa tarehe moja Julai mwaka 1895.

❹ Mbali na historia yake, uhusiano kati ya Kenya na nchi zingine umeletwa na kuwepo kwa ngome hii. Kando na hilo, uhusiano wa kihistoria umekuwepo kati ya Kenya na Ureno kwa sababu ngome inaashiria kuwepo kwa wananchi wa taifa hilo katika nchi hii. Aliyeichora ramani ya ujenzi ya Fort Jesus alikuwa ametoka Italia, hivyo basi uhusiano kati ya nchi yake na Kenya umekuwepo tangu jadi pia.

❺ Kwa watu wa pwani, kuwepo kwa jumba hili kunaonyesha uwezo wao wa kupigania uhuru. Lugha ya Kiswahili nayo imebeba maneno kadhaa yaliyotolewa moja kwa moja kutoka katika lugha ya Kireno. “Jemedari” linalomaanisha mkuu wa jeshi, “mvinyo” lililo na maana ya pombe na “bendera” ni kati ya maneno hayo. Hivyo basi, Fort Jesus ina umuhimu mkubwa katika historia ya pwani na Afrika Mashariki kwa jumla.

Imetoholewa kutoka www.jestina-george.com (2012)

https://xtremepape.rs/

**Kifungu B**

# Kwa nini kuwekeza kwenye maji na usafi wa mazingira?



❶ Watanzania wote wana haki ya kuishi kwenye hali ya usafi na kupata maji safi. Hata hivyo hali imekuwa ni ya kutisha kutokana na ukosefu wa maendeleo katika kuboresha upatikanaji wa vitu hivi muhimu sana kwa wananchi wote. Kasi ya kuboresha hali ya usafi ni ndogo sana na kwa upande mwingine juhudi za upatikanaji wa maji salama, wakati mwingine zinazidi kudorora. Hali hiyo imekuwa chanzo cha magonjwa, ulemavu, utapiamlo na vifo vya watoto, na pia imeathiri maendeleo ya taifa. Kwa kiasi kikubwa maafa haya yanazuilika, tena kwa gharama ndogo.

❷ **Sababu kuu ya magonjwa, ulemavu na vifo:**
Uchafu husababisha takribani theluthi moja ya vifo vya watoto wa umri wa chini ya miaka tano – kwa wastani, kiasi cha vifo vya watoto 130 kila siku. Vifo hivyo hutokana na magonjwa ya kuharisha na magonjwa yanayoambukizwa kwa njia ya hewa ambayo kwa kawaida uambukizaji wake hupitia mikono michafu na uchafu mwingine wa mwili wakati wa kujifungua. Ugonjwa wa kuharisha ukirudia mara kwa mara husababisha utapiamlo unaodumaza ukuaji na maendeleo ya watoto na kuathiri uwezo wao wa kufanya vizuri katika masomo shuleni. Pia uchafu ni chanzo kikuu cha upofu unaosababishwa na trakoma*.

❸ **Ongezeko dogo la matumizi ya vyoo bora:**
Idadi kubwa ya Watanzania (kiasi cha milioni 40) hawatumii vyoo bora – yaani vyoo vya kuvuta maji au vya shimo vinavyoweza kusafishwa na kutunzwa viwe safi. Pamoja na kwamba usafi wa mazingira unaweza kuokoa maisha, jambo hilo bado si moja ya vipaumbele vya serikali. Halikuingizwa katika mpango wa malengo makubwa wa sasa kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa maji na sera ya usafi wa mazingira imesubiri kwa miaka mingi bila kupitishwa.

❹ Takribani Watanzania milioni 6.5 bado hawatumii vyoo na kwa mujibu wa Benki ya Dunia, jambo hili peke yake husababisha upotevu wa karibu dola za Kimarekani milioni 46 kila mwaka nchini Tanzania. Kila mtu ambaye hana choo huweza kutumia hadi siku 2.5 kwa mwaka akitafuta tu mahali pa kujisaidia. Wanawake katika familia maskini zaidi hubeba mzigo mkubwa zaidi wa gharama hizi kwa vile pia hutumia muda wa ziada kusindikiza watoto wao, wanafamilia wagonjwa au vikongwe kujisaidia. Ili kufuta desturi hiyo inabidi kujenga vyoo vya ziada milioni moja na kuvitumia.

Imetoholewa kutoka www.unicef.org (2013)

---

* trakoma: ugonjwa hatari wa macho



https://xtremepape.rs/

**Kifungu C**

# Chanzo cha kukua na kusambaa kwa simu-mkononi Afrika Mashariki

❶ Mtandao wa simu-mkononi ulianza kupata mashiko yake katika Afrika Mashariki mwishoni mwa miaka ya 1990, wakati ambapo serikali za Uganda, Tanzania na Kenya zililegeza udhibiti wa vyombo vya mawasiliano na kuziruhusu kampuni za kibinafsi kuanzisha huduma ya simu-mkononi. Ingawa makala haya hayajadili mchakato uliozifanya serikali hizi zilegeze sera zake kuhusu huduma za simu, ni muhimu kusema kwamba mabadiliko haya yalitokea wakati ambao mtandao wa kompyuta na tovuti katika Afrika Mashariki pia viliibuka.

❷ Mabadiliko haya ni sehemu ya mabadiliko ya kiteknohama ambayo yalikuwa yanaukumba ulimwengu wote, ila kabla ya kipindi cha miaka ya 1990, yalikuwa yamefungiwa kusambaa Afrika kwa sababu nyingi. Mojawapo ikiwemo siasa zilizodhibiti vyombo vya habari ili kuzuia elimu na mawazo ya kimapinduzi kuufikia umma wa kawaida. Kutokana na hali hii, ni wananchi wachache sana ambao walikuwa na uwezo wa kutumia mtandao wa tovuti kwa kompyuta au simu-mkononi hadi mwisho wa miaka ya 1990.




❸ Sura hii ya mtandao wa mawasiliano ya simu ilibadilika kwa kasi sana baada ya serikali za Uganda, Tanzania na Kenya kubadilisha sheria ya kudhibiti nyenzo za mawasiliano ya simu na kutoa leseni kwa makampuni binafsi yaliyoanza kutoa huduma ya simu-mkononi. Kuanzia mwaka 2000 mtandao wa mawasiliano ya simu umepanuka kwa kasi ambayo ilipiku matarajio ya washika dau wote wa sekta hii.

❹ Hadi miaka ya 1990, vyombo vyote muhimu vya mawasiliano kama simu, redio na televisheni vilimilikiwa, au kudhibitiwa na serikali, kwa kuhodhi idhaa za kurushia matangazo. Mojawapo ya sababu kubwa iliyosababisha udhibiti wa vyombo hivi ni athari ya siasa za vita-baridi pamoja na sera za kidikiteta zilizotawala nchi za Afrika katika kipindi hicho.

❺ Kwa sababu nchi za Afrika Mashariki za baada-ukoloni zilijikuta katika njia panda ya kuegemea ama mrengo wa Kimagharibi (Kenya na Uganda) au wa Kimashariki (Tanzania); nchi hizi ziliendeleza sera za kutoaminiana kisiasa, kiuchumi na kiusalama. Katika hali hii, vyombo vya habari vilidhibitiwa na serikali kama njia mojawapo ya kuchuja elimu na usambazaji wa itikadi za Kimagharibi kwa wananchi wa Tanzania, na zile za Kimashariki kwa wananchi wa Kenya na Uganda.

Mahiri Mwita, www.academia.edu (2011)

https://xtremepape.rs/

**Kifungu D**

# Sheng inaharibu Kiswahilii

❶ Sheng ama lugha simo ni lugha inayotumiwa na watu wa kundi maalum kwa ajili ya kutaka waelewane wao kwa wao na pengine kuwatenga watu wengine. Katika muktadha huo ni sawa kusema kuwa ni lugha isiyokuwa na mfumo rasmi wa sarufi kwani watu hubuni majina wanavyofikiria.

❷ Majina yanaweza kubuniwa kutoka kwa vipande vya lugha tofauti, kubadilisha maneno kwa mfano kutoka nyuma ukirudi mwanzo na kadhalika. Kwa mfano, neno bata, unaweza kuwasikia vijana wa Kenya wakisema taba na kuoga wanasema kugao.

❸ Nimeanza na maelezo hayo kuonyesha namna lugha hiyo inayotajwa kuwa ya kihuni na baadhi ya wasomi wa Kiswahili inatofautiana kutokana na mtu anachosema na mahali anaposemea. Hata hivyo, kwa wataalamu wa isimu jamii watakupiga mawe ukikashifu matumizi ya sheng. Wengine hata wamefanyia utafiti kipengee hicho.

❹ Ingawa kuna mvutano mkubwa kuhusu matumizi ya sheng ama lugha simo, ni muhimu kutaja kuwa kuna baadhi ya maneno yaliyoanza kama sheng na yakaswahilishwa. Kwa mfano nchini Kenya, matatu ni magari ya uchukuzi wa umma ama matwana kwa Kiswahili sanifu. Vivyo hivyo, Tanzania chombo hicho kinaitwa daladala ambalo si jina la Kiswahili sanifu lakini limetiwa katika matumizi.

❺ Hata hivyo, kuna hasara kubwa ya kutumia baadhi ya majina ya sheng ambayo yanapotosha maana halisi ya maneno hayo ya Kiswahili. Kwa mfano nchini Rwanda mtu akiwa hajakamilika kwa namna moja au nyingine watu wanamuita kasorobo. Kwa hakika kasorobo ni neno la Kiswahili linalomaanisha kuna upungufu wa robo ya kitu kujalizia mahali fulani kama vile dakika 15 za saa na kadhalika.

❻ Sheng inapotumika katika mazungumzo inawakanganya Waswahili. Si hayo tu, Burundi ndio kuna mambo, eti muasi kwa lugha ya **[ – X – ]** ya huko ni msichana mrembo. Kwa Kiswahili **[ – 38 – ]** muasi ni mwanamgambo **[ – 39 – ]** mtu msumbufu tu asiyeambilika **[ – 40 – ]** kusemezeka. Kenya na Tanzania ni nchi ambazo zinajulikana pia kuibuka na misimo mbalimbali na inayopotosha maana halisi ya maneno ya Kiswahili.

Imetoholewa kutoka www.bbc.com (2012)

https://xtremepape.rs/